# Wanamtandao wa MJUMITA walivyodai haki yao kwa mwenyekiti wa kijiji

***Na: Mwandishi wetu Kigoma***

Ilikuwa ni tarehe 20/4/2012 siku ambayo mwenyekiti wa kijiji cha SIBWESA kilichopo katika wilaya ya Uvinza, mkoani KIGOMA alipomkataza Mratibu wa MJUMITA wa kanda ya magharibi kukutana na wana mtandao wa mtandao wa MGOBOHI ambapo lengo kubwa lilikuwa ni kutambulisha mradi wa Haki katika misitu Mwenyekiti alidai kuwa MJUMITA haijulikani na pia ni shirika ambalo halijasajiliwa hivyo hataki liendeshe shughuli zake kijijini kwake lakini wakati anadai hayo alishapokea barua kutoka kwa mkurugenzi kupitia kwa Afisa misitu wa wilaya.

Wanamtandao MJUMITA waliandamana ndani ya ofisi yake wakimshinikiza wanadai haki yao ya msingi ya kuujua mradi baada ya kuleta vurugu kubwa ya kama lisaa na nusu Mwenyekiti aliruhusu Mratibu kukutana na wanamtandao na kwa masharti baada ya hapo mratibu aongee na wana kijiji wote kwenye mkutano wa hadhara ili awaeleze wananchi kuhusu MJUMITA.Tukiwa kwenye mkutano wa ndani na wanamtandao waliweka wazi kuwa mwenyekiti anapiga MJUMITA vita kwa sababu aliahidi wananchi ya kuwa akipata uongozi ataruhusu waendeshe shughuli zao kwenye msitu wa Mgobohi, pia wapiga kampeni wake wanaendesha shughuli zao msituni ambazo ni kuchoma mkaa na kupasua mbao na wanachama wa MJUMITA wanapingana na uharibifu wa mazingira ndo maana hataki kusikia MJUMITA kijijini hapo.

Wanamtandao walifichua maovu yote ya mwenyekiti wao anavyoipinga kamati ya mazingira ambayo imejaa wanamtandao wa MJUMITA, mratibu aliripoti kwa diwani na katibu kata kuhusu suala la mwenyekiti ambalo limepelekwa wilayani kushughulikiwa na tunasuburi kuona juhudi zinafanyika kuunusuru msitu wetu wa Mgobohi. Hongereni wanamtandao wa MJUMITA, Mgogohi kwa kuitambua haki yenu.

Kazi niliyoenda kufanya ni kuutambulisha mradi wa Haki katika Misitu Tanzania, ambao unatekelezwa na shirika lisilo la kiserikali (MJUMITA), mradi ambao unashughulika na kuboresha utawala bora na uwajibikaji katika sekta ya misitu Tanzania, utafiti mdogo wa kuangalia hali ya utawala bora ulitakiwa kufanyika ambapo watu wawili kutoka kila kijiji walitakiwa kushiriki kikamilifu kufanya dodoso la utawala bora kutoka kwa wana mtandao wa MJUMITA kijiji cha Sibwesa ambao watatekeleza zoezi hilo na kurudisha majibu.

# Wanamjumita kilwa 'wamrarua' mwekezaji

Viongozi wa Kijiji watuhumiwa kulainishwa kwa Posho ya shs 5000.

***Na mwandishi wetu***

WANACHAMA wa Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) Wilayani Kilwa Mkoani Lindi wamefanikiwa kusitisha utoaji wa ardhi ya kijiji chao kwa muwekezaji ambae alionekana kutaka ardhi bila ya kufata taratibu. Muwekezaji huyo kutoka China



*Mwanachama (aliyesimama) wa mtandao wa MWATUKI, wilayani Kilwa akichangia hoja katika mkutano wa mtandao huo uliofanyika Kijiji cha Ruhatwe October 2010. Hoja kuhusu madhara ya uwekezaji usiofuata taratibu ziliibuliwa katika majadiliano hayo.*

alilenga kupata zaidi ya hekta 10,000 za ardhi bila kufuata taratibu halali katika kijiji cha Kikole. Mwekezaji huyo alidaiwa kuomba ardhi kwa ajili ya shughuli za kilimo cha mahindi na mihogo.

Maombi ya mwekezaji huyu yalitupiliwa mbali na wanakijiji walioshiriki mkutano mkuu wa kijiji katika kijiji hicho uliyokuwa imeitishwa na serikali ya kijiji hicho kwa lengo la kuwaomba wanakijiji kuridhia maombi hayo.

Mwekezaji huyu anadaiwa kutua katika kijiji cha Kikoke mnamo tarehe 18/8/2011 na barua na maelezo ya maombi ya ardhi yaliyosheheni mapambo na ushawishi kabambe uliolenga kuwalainisha wanakijiji ili wampokee kwa shangwe. Katika barua yake hiyo, mwekezaji alidai kuwapatia wanakijiji ajira na hudumba mbalimbali za jamii endapo watampa ardhi. "Uwekezaji huu utatoa ajira kwa wananchi wa kijiji chako na hivyo kuwaongezea kipato na chakula". Ilisomeka sehemu ya barua hiyo na kuongeza, "Pamoja na kufanya shughuli za kilimo kampuni yetu itatoa kipaumbele katika kuboresha miundo mbinu ya huduma za jamii kama vile shule, vituo vya afya, maji na mengine kadiri ya mahitaji ya kijiji".



Aidha, katika kile kilichoonekana kujenga mazingira ya rushwa, mwekezaji huyo alidai kugaramia gharama za mikutano itakayolenga kufanikisha zoezi hilo. "Kampuni yetu pia ipo tayari kulipia gharama ya vikao husika vya kijiji uwezesha mchakato huu na itagharamia upimaji wa eneo husika ili kubainisha mipaka yake ikiwa na nia yakuepusha migogoro katika siku za usoni" ilisema barua hiyo ambayo pia nakala yake ilipelekwa kwa afisa ardhi wa wilaya. Taarifa za ndani ya vikao vya serikali ya kijiji na mwekezaji huo zilithibitisha kuwa baadhi ya viongozi wa serikali ya kijiji walikubali kumsaidia mwekezaji huyo kuwashawishi wanakijiji wenzao ili wakubali maombi yake.

Baadhi ya wanachama wa MJUMITA wazalendo wa kijiji hicho walipopata taarifa za ujio wa mwekezaji huyo waliwaelimisha wanakijiji wenzao kuhusu madhara ya uwekezaji kwa kutumia mikanda ya video inayoonesha madhara hayo. Huku wengine wakipita mtaa kwa mtaa na nyumba kwa nyumba, kuwahamasisha wenzao kuhudhuria mkutano mkuu utakaoitishwa ili kwenda kusitisha hatua zozote za muwekezaji huyu kuchukua ardhi yao.

Katika mkutano mkuu ulioitishwa kijijini hapo tarehe 26/08/2011, mwekezaji huyo alipata wakati mgumu kujibu hoja za wanakijiji, likiwepo swala la kutoa posho kwenye vikao vya serikali ya kijiji isivyo kawaida na kuhojiwa ni kwanini kama wana fedha wasitoe posho kwenye mkutano mkuu wa kijiji pia. "Hatukuambiwa kama kuna utaratibu wa posho/chakula kwenye mkutano kama huu na hivyo hatukujua tuandae kiasi gani..." alisikika mwakilishi wa kampuni hiyo akilalamika mkutanoni.

Aidha waliohudhuria mkutano huo walipinga kwa nguvu zote na kuitahadharisha serikali ya kijiji kuhusu madhara ya uwelezaji wa namna hiyo ulivyoathiri vijiji vya jirani. Hata hivyo kampuni hiyo inadaiwa kuendelea kuhaha kutafuta maeneo katika vijiji vingine katika wilaya ya Kilwa na taarifa ambazo hazijathibitishwa zinasema kuwa wameshafanikiwa kupata hekta kadhaa katika vijiji jirani.

Mwekezaji huyo alidaiwa kuomba ardhi kwa ajili ya shughuli za kilimo cha mahindi na mihogo